**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**664** **MITAALA NA UFUNDISHAJI**

**Muda: Saa 3.** **Wednesday, 14th Mei 2008**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu **B** na swali **moja (1)** kutoka sehemu **C**.
3. Sehemu **A** ina alama 36, sehemu **B** ina alama 40 na sehemu **C** ina alama 24.
4. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (alama 36)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha vipengele vinne (4) muhimu vinavyopaswa kuwepo katika mtaala wa shule.
2. Taja na fafanua kwa ufupi njia tatu (3) za kufundishia zinazomfanya mwanafunzi kuwa kiini cha ujifunzaji.
3. Kwa nini ni muhimu kwa mwalimu kuandaa zana anazohitaji kabla ya kuingia darasani?
4. Eleza dhana ya malengo ya jumla na malengo mahsusi katika mitaala.
5. Orodhesha hatua nne (4) za kuandaa azimio la kazi.
6. Taja aina tatu (3) za tathmini zinazofanyika katika mchakato wa ufundishaji.
7. Fafanua maana ya njia ya ugunduzi kama mbinu ya ufundishaji.
8. Tofautisha kati ya mtaala uliopangwa na mtaala uliotekelezwa.
9. Orodhesha milango ya maarifa **ya mwanafunzi** mitano (5) inayozingatiwa katika ufundishaji.

**SEHEMU B (alama 40)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii.

10. Jadili namna mazingira ya shule yanavyoweza kuathiri utekelezaji wa mtaala.
11. Fafanua faida nne (4) ambazo mwanafunzi anapata anapopewa fursa ya kujitathmini mwenyewe.
12. Chagua somo lolote katika shule ya msingi kisha andika malengo matatu (3) ya somo na shughuli za kufundishia na kujifunzia zinazolingana na malengo hayo.
13. Eleza kwa kina namna kutoandaa andalio la somo kunavyoweza kusababisha ufundishaji usio na mpangilio mzuri.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU C (alama 24)**

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

14. Jadili mikakati mitano (5) anayoweza kutumia mwalimu kukabiliana na wanafunzi wenye viwango tofauti vya uelewa darasani.

15. Fafanua namna kuhakiki mazoezi ya wanafunzi kunavyoweza kumsaidia mwalimu kujitathmini.

16. Eleza umuhimu wa mtaala kuwa na sifa ya unyumbulifu katika muktadha wa elimu ya kisasa.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org